



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

WAOMBAJI WALIODAHILIWA ZAIDI YA CHUO KIMOJA KATIKA AWAMU YA TATU YA UDAHILI NA AWAMU ZILIZOPITA KWA MWAKA WA MASOMO 2020/2021

Dar es Salaam, 10 Novemba, 2020

1.0 UTANGULIZI

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma na wadau wa Elimu ya Juu nchini kuwa Awamu ya Tatu na ya mwisho ya udahili katika Taasisi za Elimu ya Juu, ngazi ya Shahada ya Kwanza kwa mwaka wa masomo 2020/2021 umekamilika. Majina ya waombaji waliodahiliwa katika ***Awamu ya Tatu*** yametangazwa na vyuo husika.

2.0 WAOMBAJI WALIODAHILIWA KATIKA CHUO ZAIDI YA KIMOJA


Waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika Awamu ya Tatu na wale wa awamu zilizopita ambao bado hawajathibitisha udahili, wanasisitizwa kuthibitisha udahili wao katika chuo kimojawapo kuanzia leo tarehe 10 hadi 15 Novemba, 2020. Uthibitisho huo ufanyike kwa kutumia ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri uliotumwa kupitia namba zao za simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kuweza kujithibitisha katika chuo ambacho muombaji anakipenda.

Aidha, uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti ambayo muombaji alitumia wakati wa kuomba udahili katika chuo alichokichagua. Orodha ya majina ya waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika Awamu ya Tatu na wale wa awamu zilizopita ambao bado hawajajithibitisha imewekwa kwenye tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

3.0 WITO KWA WAOMBAJI UDAHILI

Waombaji udahili wa Shahada ya Kwanza wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusu udahili au kujithibitisha katika chuo kimoja yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika. Kwa wale ambao watapata changamoto katika kujithibitisha, vyuo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka.

Imetolewa na:



Prof. Charles D. Kihampa
KATIBU MTENDAJI
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA